

# Mafuriko na magonjwa yanayoenezwa na mbu

Taarifa kuhusu jinsi ya kuzuia magonjwa yatokanayo na mbu baada ya mafuriko au mvua kubwa

Swahili | Kiswahili

## OFFICIAL

Baada ya mafuriko au mvua nyingi, mbu hukua na kuenea katika madimbwi ya maji yaliyoachwa nyuma. Mbu wanaweza kubeba magonjwa na kuyaeneza kwa kukuuma.

### Njia bora ya kuzuia magonjwa yanayoenezwa na mbu ni kuepuka kuumwa na mbu!

Magonjwa yanayoenezwa na mbu huko Victoria ni pamoja na virusi vya Ross River, Barmah Forest Virus, Murray Valley Encephalitis (MVE) na virusi vya encephalitis ya Japani (JE). Virusi vya JE na MVE vinaweza kusababisha ugonjwa mbaya na kifo kwa baadhi ya watu. Chanjo ya JE inapatikana bila malipo kwa watu mahususi, wasiliana na daktari wako ikiwa wewe unastahili. Maelezo zaidi kuhusu chanjo ya JEV yanaweza kupatikanahapa.

### Jilinde dhidi ya kuumwa na mbu!

- Jufunike Vaa nguo ndefu, zisizobana na za rangi zenye kungaa.
- Tumia dawa za kufukuza wadudu ambazo zina picaridin au DEET.
- Usisahau watoto - mda wote angalia lebo ya dawa ya kufukuza wadudu. Kwa watoto, nyunyiza au paka dawa ya kufukuza kwenye nguo zao badala ya ngozi zao. Usitumie kwenye mikono ya watoto wachanga au watoto wadogo.
- Usitoke nje ikiwa unaona mbu wengi nje, haswa jioni na alfajiri, ambazo ni nyakati za kuuma sana.
- Lala chini ya chandarua ikiwa uko nje na hujalindwa na skrini za wadudu.
- Tumia dawa ya kupuliza nzi, mizunguko ya kufukuza mbu, au dawa ya kuingiza kwenye tundu la umeme kufukuza mbu mahali unapokusanyika ili kuketi au kula.
- Mahali ambapo kuna maji yaliyotumama, epuka eneo hilo na ukae ndani ikiwezekana.

### Kuzunguka nyumba

- Ondoa maji na vyombo ambavyo mbu huzaliana pamoja na ndoo, matairi ya zamani, mabwawa ya samaki, magari ya maji ambayo hayajazibwa na vyombo vya kuweka mimea.
- Maji katika vyombo karibu na nyumba yanapaswa kumwagwa angalau mara moja kwa wiki.
- Funika madirisha yote, milango, matundu, na viingilio vingine kwa kutumia skrini za wadudu.
- Ondoa taka au mimea iliyokomaa kwenye mifereji ya maji na mikora ya maji.
- Punguza vidimbwi vya maji ndani na karibu na yadi.
- Angalia skrini ya tanki la maji kama inafanya kazi vizuri na ubadilishe skrini zilizoharibika.

### Wapi pa kupata msaada

Ikiwa una matatizo ya kiafya, muone daktari wako, au mpigie simu Muuguzi-wa-zamu kwa 1300 60 60 24. Katika hali ya dharura, piga simu 000. Kwa usaidizi mwingine, wasiliana na baraza la mtaa wako.

Ili kupokea chapisho hili katika muundo unaofikiwa, tuma barua pepe [pvh.communications@health.vic.gov.au](mailto:pvh.communications@health.vic.gov.au)

